Child Abuse & Neglect 43(2015)8–21

Orodha Yaliyomo inapatikana katika ScienceDirect

Unyanyasaji wa Watoto & Kutelekezwa

ELSEVIER

Nakala ya Utafiti

# Mbinu za kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto kuanzia chini kwenda juu mbinu na: Kuangazia watoto, familia na jamii

CrossMark

Michael G.Wessells

Chuo Kikuu cha Columbia, Marekani

article info

Historia ya makala:
Kupokea 9 Aprili 2015
Kubalika 9 Aprili 2015

Maneno:
Ulinzi wa watoto
Mifumo yenye msingi wa jamii
Umiliki wa jamii
Haki za watoto

mpasho

Juhudi za kitaifa za kuimarisha mifumo ya ulinzi wa watoto mara nyingi huwa yanachukua mkondo wa juu-chini katika kuweka mikakati kuhusu huduma rasmi za kiserikali. Mbinu kama hizi zinazoendeshwa na wataalam mara nyingi huwa na sifa za matumizi ya chini ya huduma rasmi na kutokuwa na mikakati bora katika nyanja ya sehemu rasmi na zisizo rasmi kwenye mfumo wa ulinzi wa watoto. Nakala hii inachunguza mbinu mbadala za kijamii zinazotokana na kazi inayofanyika kutokea chini kwenda juu ambazo zinawezesha huduma rasmi na zisizo rasmi kushirikiana na kuafikiana ilikuboresha matumizi ya huduma rasmi kwa ukubwa, kuleta mabadiliko ya ndani inayo endeshwa na jamii, na kiwango cha juu cha umiliki wa jamii. Mbinu kubwa zinazotegemea uongozi wa wataalam katika Kamati zinazosimamia Ustawi wa Watoto hutoa viwango vya chini vya umiliki wa jamii. Kwa kutumia mbinu iliyovumbiliwa na kufanyiwa majaribio katika maeneo ya vijijini Sierra Leone, ikiongozwa na hatua za sera ya kijamii, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na uhusiano wa mifumo rasmi ambayo inaendeleza matumizi ya huduma rasmi na mafanikio kwa kuongeza umiliki, ufanisi, na endelevu wa mfumo huo. Nyanja hii inahitaji hali ya chini ya kutegemea mbinu zinaongozwa na wataalam na matumizi ya pana sana na polepole, ikiongozwa na jamii, kutumia mbinu za kutoka chini kwenda juu katika ulinzi wa motto.

## Tangulizi

Katika dunia nzima, nyanja za ulinzi wa watoto katika mazingira ya kibinadamu inafanyiwa mabadiliko ya kihistoria ikielekezwa katika uimarishaji wa mifumo ya ulinzi wa watoto kwa kiwango cha kitaifa (Sera Mtoto wa Afrika Forum na wenzake, 2013;. Davis, McCaffrey, & Conticini, 2012; UNICEF, UNHCR, & Maono Duniani 2013;. Wulczyn na wenzake, 2010). Mbinu hii inalenga kusaidia ulinzi wa watoto kwa kina cha undani na kutoa ahadi ya kuipa nguvu juhudi za kuzuia matatizo ya unyanyasaji, vurugu, unyonyaji, na maswala ya watoto kutelekezwa. Utaratibu wa mbinu hii ni ya muhimu na ya kutia moyo, lakini changamoto nyingi zimejitokeza katika utekelezaji. Juhudi nyingi katika ramani na uimarishaji wa mifumo ya ulinzi wa watoto, umekuwa ni wa juu-chini na umeshindwa kusikiliza kwa undani kuhusu familia na jamii au kutambua vilivyo

michango yao katika ulinzi na ustawi wa watoto.

Mbinu za kina zaidi katika kuimarisha mikakati ya ulinzi wa watoto ni kuchanganya na kujumuisha kwa usawa mbinu za juu-chini, chini-juu na sehemu za katikati-nje. Mbinu za juu-chini kuhakikisha kuwa serikali iko na sheria, masharti na uwezo, ambao ni muhimu kuwalinda watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Mbinu za chini-juu zinafanya kazi kutoka ngazi za chini kwenda juu, na zinahusu hatua za kijamii, kuendeleza mikakati zilizopo za kuimarisha na kuvutia ushirikiano wa jamii na serikali. Mbinu za Katikati-nje, ambazo zinatokana na wadau kama vile mabaraza ya miji ilioko katikati ya ngazi za kitaifa na za mashinani, zinaendeleza ajenda ya ulinzi wa watoto katika vituo vya uongozi katika mikoa. Mbinu hizi tatu ni nyongeza.

## Mifumo ya ulinzi wa watoto

Katika mazingira ya kibinadamu, watoto wanakabiliwa na hatari kama vile kutengwa na walezi, vurugu za kifamilia, unyanyasaji wa kijinsia na unyonyaji, ulemavu, vurugu katika shule na jamii, ndoa za mapema, masuala ya haki, kuishi na kufanya kazi katika mitaa, kazi za hatari, ulanguzi, ugonjwa wa ukimwi, na kukosa uwezo wa kukidhi mahitaji ya kimsingi. Kabla ya ujio wa mifumo ya kuimarisha katika mwaka wa elfu mbili na nane mashirika mengi yasio ya kiserikali na wahudumu wa maendeleo walilenga kulinda miradi ya makundi maalum ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Matokeo yake yalikuwa ni miradi uliyosambaratika na kushindwa kuwajibika kwa ajili ya changamoto zilizokabili watoto (kwa mfano, mtoto ambaye leo alikuwa akiishi mitaani siku nyingine angeweza kuwa mwana jeshi mwenye umri mdogo; Wessells, 2006; Zack-Williams, 2013). Na pia, nyanja za kulinda watoto ilikuwa imeelezeka kupita kiasi katika masuala ya jitihada za ulinzi wa watoto na kutoshugulikia sana katika uzuiaji. Mabadiliko haya ya dhana kuelekea katika mifumo ya ulinzi mtoto inatumika sehemu kwa kiasi kama marekebisho katika upungufu huo na inatambua kuwa masuala ya utaratibu huo unahitaji mbinu za utaratibu zilizo sawa.

### *Mifumo ya ulindaji wa watoto ni nini?*

UNICEF(tazama UNICEF et al., 2013) inaelezea mifumo ya ulinzi wa watoto kama " mambo fulani rasmi na miundo isiyo rasmi, majukumu na uwezo ambazo zimekusanywa ili kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji, dhuluma, kutelekezwa, na unyonyaji wa watoto" (p.3). Vipengele vya msingi wa mifumo ya ulinzi wa watoto ni pamoja na sheria na sera, rasilimali ya watu na fedha, uwongozi bora, njia ya ukusanyaji wa takwimu na mfumo wa ufuatiliaji, ulinzi wa watoto na huduma za kukabiliana na misaada ya familia na jamii isiyo rasmi.

Watendaji mbalimbali wanajumuisha mfumo ya ulinzi wa watoto. Watendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali wanabeba jukumu la msingi kwa ajili ya

ulinzi wa watoto ndani ya mipaka ya nchi. Watendaji rasmi kama vile viongozi wa ustawi wa jamii, polisi, wafanyikazi wa kijamii serikalini, na mahakimu huongoza mfumo wa ulinzi wa watoto katika ngazi za kitaifa na mikoa.

Katika mashinani, jukumu la watendaji wasiyo rasmi inaonekana sana. Kama ilivyo katika mifumo ya kijamii mazingira ya maendeleo ya mtoto (Bronfenbrenner, 1979; Dawes & Donald, 2000), ulinzi wa watoto mara nyingi huwa chini ya watendaji wasiyo rasmi kama vile familia, jamii, na viongozi kama vile wazee, walimu, au viongozi wa dini. Katika ngazi za jamii, vyombo vya habari, viongozi wa serikali, na mashirika ya kiraia wana jukumu muhimu. Kwa sababu matatizo kama vile ulanguzi wa watoto, shirika la kimataifa la msalaba wa mipaka na watendaji wa kimataifa pia huchangia au kusaidia mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa watoto.

Mifumo ya ulinzi wa watoto ni urithi unaojumuisha mambo mbalimbali na sekta tofauti. Ingawa ulinzi wa watoto tangu hapo miaka ya jadi ilikuwa ikionekana kama jambo la wizara ya ustawi na kijamii na wadau kama vile polisi na mahakimu na sekta nyingine zina jukumu muhimu katika kulinda watoto (Kikundi cha kazi ya Ulinzi wa Watoto, 2012). Kwa mfano, ushiriki katika elimu mara nyingi hulinda watoto kutokana na kuangazwa kwenye madhara mengine kama vile unyanyasaji wa ngono au madawa ya kulevya (Wessells, 2011; Wessells, Kostelny, na Ondoro, 2014). Vile vile, wahudumu wa afya mara nyingi huwa hudumia watoto waliodhulumiwa au watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa sababu ya masuala ya afya kama vile ukimwi na ulemavu. Usajili wa uraia ni muhimu kwa sababu watoto wasio na usajili rasmi wa serikali wako katika hatari ya ubaguzi na kukosa uwezo wa kupata huduma ya msingi ya afya na huduma nyingine. Sekta ya uchumi, pia, iko na ushawishi mkubwa maana umaskini mara nyingi huchangia hadhari za ulinzi wa watoto na pia inaathiri mambo ya kinga katika ngazi mbalimbali (Collier et al 2003). Kwa sababu hizi, mifumo ya kuimarisha ulinzi wa mtoto inahitaji mbinu pana kana kwamba kuyazuia migawanyiko makubwa kati ya sekta ambazo zinahusika na usanifu wa mambo ya kibinadamu.

Watendaji wasiyo wa kirasmi - wakiwemo watoto, familia, na jamii - ni sehemu muhimu ya mifumo ya ulinzi wa watoto, ingawa mara nyingi muno wanaagaziwa kama wenye kunufaika au pia kama wenye kukumbwa na matatizo. Watoto huonyesha ujasiri mkuu huku kukiwa na mashaka (Boothby, Strang, & Wessells, 2006; Fernando & Ferrari, 2013; Panter-Brick & Leckman, 2013; Ungar, 2008), kupitia mazingira magumu, na kushiriki katika ulinzi wa kibinafsi. Watoto ni watendaji wa kijamii na kisiasa ambao wanaweza kusaidia wenzao, familia na jamii kuwalinda watoto. Ingawa wazazi wanaweza kosa kutaja "ulinzi wa watoto" kama shughuli yao, wao hufanya mengi katika kuwalinda watoto kutokana shughuli za kawaida kama vile kuwazuiza watoto wachanga kutokana na madhara, na kuwafundisha watoto tabia nzuri na jinsi ya kuepuka hatari. Jamii hujumuisha pamoja rasilimali za thamani katika ulinzi kama vile viongozi wa dini, walimu, wazee, wauguzi, na wasaidizi wa kiasili

ambao hukabiliana na kuzuia madhara kwa watoto. Ili kuwa na uhakika, watoto, familia na jamii wanaweza pia kuwa wahusika wa ukiukaji wa haki dhidi ya watoto. Familia mara nyingi huwadhuru watoto kwa njia kama vurugu za kifamilia au unyanyasaji wa kijinsia, na jamii hutumia mazoea yenye madhara kama vile ukeketaji wa wanawake. Matatizo haya, hata hivyo, hayapaswi kukata makali ya nia yetu kwa majukumu makuu kuhusu watoto, kama vile familia na jamii hushiriki katika mifumo ya ulinzi wa watoto.

## Utaratibu wa kijamii kwa kuwalinda watoto

Utaratibu wa kijamii kwa kuwalinda watoto (CBCPMs) ni makundi ya kawaida au taratibu ambazo hujibu kwa ukiukaji dhidi ya watoto na hufanya kazi ili kuzuia hatari kwa watoto. CBCPMs ni sehemu muhimu ya mifumo ya ulinzi wa watoto kwa vile zinafanya kazi mashinani kama vile ngazi ya kijiji katika maeneo ya mashambani na mitaani katika maeneo ya mijini, hapa ndipo watoto na familia huishi na ambapo watoto wanaweza kuwa exposed/wazi kutokana na hadhari kubwa katika misingi endelevu. Pia, kuna uwezekano mkubwa wa rasilimali za ulinzi wa watoto kama vile wazazi, walimu, na viongozi wa dini, miongoni mwa wengine.

Mashsirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali mara nyingi husaidia kuanzisha Kamati za Ustawi wa Watoto (CWC) au Kamati za Ulinzi wa Mtoto zitakazo kuwa na wanawake 10-20 na wanaume na pia watoto. Kwa kuwa wamepata mafunzo, Kamati hizi hufuatilia, hushawishi, hupunguza, na kuzuia aina mbalimbali za unyanyasaji wa watoto. Katika mazingira ya dharura inasaidia watoto wamekuwa wadhaifu au wamevunja vunjwa mioyo. CWC ni mmoja wapo ya hatua nyingi za kuingilia kati hutumika kwa ulinzi wa mtoto. CWC pia kutumika mara nyingi katika mazingira ya mpito na maendeleo kwa mrefu.

Ingawa hizi taratibu za nje wameanzisha ni za muhimu, ni kosa kuwadhania wao kama wataalamu wa kijamii wa kuwalinda watoto kuwa washirika wakuu. Jamii mara kwa mara huwa na taratibu za kindani ambazo zinafanya kazi kienyeji, bila uwezeshaji au uongozi kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali au serikali. Wanaweza kutekeleza majukumu ya ulinzi wa watoto ingawaje jina haijaorodheshwa vikamilifu katika shuguli kama hizo. Kwa mfano, katika Kusini mwa Afrika, ambapo idadi kubwa ya watoto wamekuwa mayatima kutokana na virusi vya ukimwi, vikundi vya kidini vilipanga usaidizi kwa mayatima (Donahue & Mwewa, 2006; Foster, 2004). Vile vile, kule Sierra Leone, machifu na wazee wa vijiji mara nyingi husaidia kutatua migogoro baina ya familia juu ya majukumu ya mvulana au mwanaume ambaye amepachika msichana mimba (Wessells, 2011). Kama CBCPMs wanapata usaidizi kutoka nje au wanajimudu, hawapaswi kupigiwa pato. Kwa kweli, kuna sababu muhimu kwa kila mmoja,kuhusu zote mbili kwa kiasi cha kuridhisha na kufahamu.

*Maswali muhimu*

Matatizo makubwa ya kiasili katika kazi ya ulinzi kuwa kwa hatari ya kukiuka Hali ya Kutokuwa na Madhara ni muhimu kuuliza maswali muhimu kama vile yafuatayo.

– Je, mifumo ya ulinzi wa mtoto inayoendeshwa na serikali ni ya miundo ya kikoloni?
– Ni kiwango gani yenye masuala rasmi ya mfumo wa ulinzi wa mtoto inafaa kuingizwa katika mazingira ya wenyeji? Je, wao hujenga juu au kutenga mbinu zilizopo au taratibu?
– Katika ngazi za chini/mashinani, je ni kweli watu hutumia njia rasmi wakati kesi kubwa za unyanyasaji wa watoto hutokea, au wao hutegemea usaidizi wa familia na jamii?
– Ni utaratibu upi wa mambo yalio rasmi na yasiyo rasmi kwenye mifumo ya ulinzi wa watoto?
– Ni kiwango gani cha ufanisi na endelevu wa kijamii katika taratibu za ulinzi wa mtoto?
– Je, kuna uwezekano wa kuimarisha juhudi za kuwalinda watoto katika ngazi ya jamii kupitia shuguli zinazo endeshwa na jamii?

Katika kuendeleza mazingira, mifumo ya ulinzi wa watoto kitaifa mara nyingi huingiani vibaya na mazingira ya ndani kwani yameundwa kulingana na misingi ya nchi zilizo upande wa Kaskazini wa dunia (Krueger, Thompstone, & Crispin, 2013). Kama serikali au mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa yataweka mifumo inayozingatia maadili ya nje na kujenga kutofatilia taratibu zilizopo, wenyeji wana uwezekano wa kutumia taratibu zisizo rasmi,na kwamba wakati mwingine huzua mgogoro ya masuala rasmi ya mfumo. Matokeo ya mfungamano yalio rasmi na yasio rasmi huzuia, uratibu na uangalifu na inahitajika kwa ajili ya mfumo wa kufanya kazi kwa ufanisi.

Katika ngazi ya jamii, swali tatanishi imekuwa kama CWC wana ufanisi na endelevu. Pia swali ni, ni vipi raia watakubali kutumia CWC zinazo endeshwa na kuanzishwa na wataalam wa mashirika yasiyo ya kiserikali au serikali. Maswali hayo yalisababisha watendaji mbalimbali wa ulinzi wa mtoto kufanya tathmini ya kimataifa ya CBCPMs mwaka 2009, matokeo yake ambayo ni muhimu hadi wa leo.

## Mapitio ya mashirika ya kidunia kwa pamoja ya CBCPMs

Mapitio ya CBCP yaliongozwa na Kumbukumbu la Kundi la mashirika yasiyo ya kiserikali, Umoja wa Mataifa na mashirika ya misaada ambazo zilifanya kazi katika ulinzi wa watoto. Kikundi hiki cha Kumbukumbu kiliratibiwa na Save the Children na ilishirkisha pamoja mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo mara

nyingi yalisaidia kuanzisha CWCs katika mazingira ya kibinadamu. Mapitio haya yalichunguza machapisho 160, nyingi zao zikiwa ripoti tatanishi zilitathmini CBCPMs hasa katika bara la Afrika na Asia (tazama Wessells, 2009a). Ripoti hizi zilishirikisha kwa pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwezeshwa na CBCPMs katika taratibu zilizo za undani, na idadi ndogo ya tathmini za kitaalam kutoka sekta ya afya zinazo husiana na watoto walioathirika na virusi vya ukimwi.

Mapitio haya yalipata udhaifu wa msingi kuhusu CBCPMs. Tathmini nyingi zilikosa miundo imara, zilifanyika mfupi baadaye bila hatua za msingi, na hawakujumuisha hali ya kulinganisha ambayo ni muhimu kwa kufikiria ni kawaida kuhusu ufanisi wa CBCPMs. Tathmini zaidi zililenga viashiria mchakato na pato badala ya matokeo kwa watoto na familia. Kwa sababu hizi, mapitio hii ilitia wito wa haraka kwa tathmini zaidi zenye utaratibu na umakini kuhusu matokeo halisi kwa watoto.

Mapitio ilitambuwa mambo saba yaliochangia katika ufanisi na endelevu wa CBCPMs: jumuiya ya kumilikii na kuwajibika; kuchanganya na kuendeleza kwa kutumia rasilimali za mitaa; msaada kutoka kwa viongozi; ushiriki halisi wa mtoto; usimamizi unaoendelea wa masuala ya nishati, utofauti, na ujumla; mafunzo ya nje na rasilimali; na uhusiano (ikiwa ni pamoja na uhusiano isiyo rasmi na iliyo rasmi) na sehemu nyingine za mfumo ya ulinzi wa watoto. Kwa sababu umiliki wa jamii ndio ulikuwa kidokezo muhimu cha kuona kama CWC ulikuwa nzuri na endelevu, inahitaji kibali ya kuwa na majadiliano ya ziada.

*Umiliki wa jumuiya*

Umiliki wa jamii inahusu wanajamii 'maana kwamba CWC au CBCPM ingine ni' yetu 'na kwamba wana nguvu na wajibu wa kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Umiliki wa jamii ni, basi sehemu muhimu ya hatua inayotokana na kuendeshwa na jamii. Umiliki mara nyingi unatambulika katika lugha ambayo watu wa ndani hutumia kuelezea CWC.

**Meza 1/Orodha 1**

Njia nne mbalimbali zakushirikiana najamiinakusababishakiwango chaushirikikwakila jamii.

| Jamii | Maelezo | Umiliki cha |
|---|---|---|
| 1 | Moja kwa moja utekelezaji na shirika: shirika ni mtoa huduma; wanajamii ni walengwa | chini |
| 2 | Ushiriki wa jamii katika mpango wakala: shirika ni mtekelezaji wa mpango wake mwenyewe, mpangaji na mkufunzi, na wanajamii ni kujitolea na walengwa | Chini ya wastani |
| 3 | Jumuiya inayomilikiwa na kusimamiwa shughuli kuhamasishwa na shirika nje: shirika ni kichocheo, uwezo wajenzi, mwezeshaji wa mahusiano, na mfadhili baada umiliki wa jamii ina maendeleo. Wanajamii ni wachambuzi, mipango, watekelezaji, wazee wa baraza, na pia walengwa | Wastani wa juu |
| 4 | Jumuiya inayomilikiwa na kusimamiwa shughuli ulianzishwa kutoka ndani ya jamii: shirika ni uwezo wajenzi na mfadhili, na wanajamii ni wachambuzi, mipango, watekelezaji, wazee wa baraza, na pia walengwa. | Juu |

Kauli kwamba "hii UNICEF au mradi wa shirika lisilo la kiserikali" zilionyesha kiwango cha chini au wastani katika umiliki wa jamii. Viwango vya juu vya umiliki vilionyeshwa na watu wakisema, "Kazi hii ni njia yetu ya kuwasaidia watoto wetu." Kisaikolojia, viwango vya juu vya umiliki wa CBCPM vilihusisha hisia ya pamoja ya wajibu uliosukuma mtu binafsi na vikundi kuhakikisha kwamba CBCPM ni madhubuti na mavuno yenye faida ya kudumu kwa watoto.

Swali muhimu ilikuwa ni kama shirika lisilo la kiserikali uwezesha CWC walikuwa na kiwango cha juu cha umiliki wa jamii kwa kuchangia ufanisi wa upeo na endelevu. Kwa sababu kiwango cha umiliki kinahusiana na jinsi vyombo vya kujihusisha na jamii, tulichambuwa tathmini hii kwa kutumia taipolojia zilizotengenezwa awali (Behnam, 2008) kuhusu hali ya mashirika yasiyo ya kiserikali katika ushiriki wa jamii.

Meza 1 inaonyesha aina nne au njia za ushiriki wa jamii. Ya kwanza ni mbinu ya huduma ya moja kwa moja, inaleta viwango vya chini vya umiliki. Kwa mfano, katika kambi ya wakimbizi ambapo watoto wanakabiliwa na hatari ya karibu sana, mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kuunda CWC wakitumia wafanyakazi ambao hupokea ripoti za matumizi mabaya au ukatili dhidi ya watoto na vile wale hujibu kupitia kwa wenye mamlaka. Mbinu hii hutumia watu katika jamii kama wamiliki na hufanya kuleta umiliki mdogo wa jamii, kwa sababu tangu hapo CWC ilipoanzishwa na kufanya kazi hawakuwa wakishirikiana pamoja na wanajamii. Aina ya 2 ni, mbinu mtaalam inayotokana ushirikiano ambao wakala wanawaza nini ifanyike, unatoa wazo kwa jamii, inakaribisha wao kushiriki kama kujitolea na walengwa, na hutoa mafunzo na ufadhili kama inavyohitajika. Kwa mfano, shirika lisilo la kiserikali inaweza kuongeza ufahamu katika jamii kwa vijijini kuhusu masuala ya ulinzi wa watoto, kupendekeza haja ya kuwa na CWC, na kuuliza jumuiya kwa mpenzi katika malezi yake, maendeleo na kazi. Jamii ingesaidia kuchagua wanachama CWC, ambaye wangejitolea kwa muda wao na juhudi. Wanajamii wangekuwa na uwezekano, uzoefu wa baadhi umiliki juu ya CWC kwa vile wao walikuwa na ushirikiano juu ya maendeleo yake na kazi. Kwa sababu wazo, utaalamu wa kiufundi, fedha, na maono ulikuja kutoka shirika lisilo la kiserikali, hata hivyo, wenyeji wangekuwa na uwezekano wa kuona mradi NGO na bila uzoefu kiwango cha juu cha umiliki wa CWC.

Aina ya 3 na 4 inahusisha nguvu kubwa ya jamii na kufanya maamuzi, na itaweza kuleta ngazi za juu wa umiliki kwa jamii. Katika aina ya 3, shirika huanzisha majadiliano kuhusu CBCPMs lakini wanahusika sana kama mtaalam na zaidi kama mwezeshaji wa mipango ya jamii na utekelezaji. Kwa mfano, shirika lisilo la kiserikali inaweza kuwezesha mazungumzo ya pamoja kuhusu jinsi ya kuwasaidia watoto walio na changamoto. Jamii yenyewe inaweza kutambua masuala muhimu na kuchukua uamuzi wa kueleza kwa kutumia Kamati tayari zilizopo, Kijiji Maendeleo, kufanya kazi kwa pamoja na vikundi vya wanawake, makundi ya kidini, na vikundi vya vijana. Kwa sababu wanajamii hufanya maamuzi na kuchukua jukumu la msingi kwa ajili ya kazi,

mbinu hii inazalisha kiasi kikubwa cha umiliki wa jamii. Aina ya 4, jamii kuanzisha na kusimamia shughuli kwa kutoka ndani, kwa msaada mdogo au bila shirika la kutoka nje. Kwa mfano, vikundi vya kanisa nchini Kenya watatenda kwa juhudi zao wenyewe kwa kusaidia watoto mayatima na watoto wengine wanaoishi katika mazingira magumu. Kwa sababu hatua hiyo inatokana na jamii wenyewe, inazalisha kiwango kikubwa cha wenyewe kuwajibika na umiliki wa pamoja.

Kati ya karatasi mia moja na sitini yaliyopitiwa, mia moja na kumi na mbili yalikuwa na maelezo ya kutosha kuhusu namna ya ushiriki wa jamii ili kuwawezesha kutofaitisha kulingana na aina. Kama Takwimu 1 inaonyesha, kubwa au utaratibu uliotumika mara nyingi zaidi kwa ushiriki wa jamii, ilikuwa aina ya 2 au mbinu ya ushirikiano. Mbinu hii ina uwezo wa kutambua kama vile wakati kuanza kwa haraka, wakati wa kujibu kwa haraka kukabiliana na madhara kwa watoto. Lakini kwa wazi inakosa viwango vya juu ya umiliki wa jamii, ambao unahitajika kwa ajili ya kufikia ufanisi upeo na endelevu. Utafiti huu unapaswa kutumika kama wito wa kuchangamsa kuhusu haja ya kujenga ngazi za juu za umiliki wa jamii katika kazi ya ulinzi wa watoto.

Mapitio pia yalitambua mambo mbalimbali ambayo yanakuza umiliki wa jamii. La msingi katika haya ilikuwa ni hisia ya uwajibikaji wa pamoja na wanajamii. Hii ilikuwa msingi katika dhamira ya kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, uwezeshaji wa pamoja, na kuwa na uwezo halisi ya kufanya maamuzi muhimu na kuongoza kazi. Kiwango cha umiliki wa jamii kilikuwa cha juu wakati watu wanatambuwa kazi kama "yetu" na kuchukua jukumu katika kuleta ufanisi wake. Kiwango cha umiliki wa jamii kilikuwa na uhaba wa mambo fulani dhidi ya mambo ya nje (kwa mfano, "Huu ni mradi wa Save the Children"), ambao ulisisitiza majukumu ya mashirika katika utendekaji wa kazi.

Umiliki wa jamii ulikuwa uti wa mgongo pamoja na uhaasishaji wa ndani wa rasilimali za jamii, hasa kwa roho ya kujitolea. Kama wazazi, walimu, wazee, viongozi wa vijana, viongozi wa dini, waganga wa jadi, na wengine walielewa




**Takwimu 1** **Asilimia ya nakala zilizochapishwa kulingana na mbinu zinazohusisha jamii.**

hisia za watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kushiriki katika masimulizi kuhusu vile 'watoto hawa wanaishi katika mazingira magumu ni wajibu wetu,' waliamua kujitolea muda wao na hutumia mitandao yao na utaalamu kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Katika baadhi ya matukio, walikusanya pesa, chakula au mavazi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, walipatiana viwanja kwa ajili ya bustani au nyumba, au sherehe ilikuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Uhusiano wa mviringo ulikuwepo kati ya uhamasishaji wa rasilimali na umiliki wa jamii. Ushiriki wa hiari wa watu kutoka nyancha mbalimbali za kazi ulisaidia katika muinuko wa hisia ya umiliki wa jamii, ambayo kwa upande mwengine uliwaongezea tamaa ya kujitolea muda wao, nguvu, na mali ili kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Kukuza umiliki wa jamii, mashirika ya nje yaliweka masisitizo ya kutosha juu ya kufanya maamuzi kwa jamii 'na kuchukua hatua kwa niaba ya watoto. Badala ya kufanya kazi kama wataalamu, wafanyakazi wao walifanya kama wawezeshaji ambao walisikiliza, wakajifunza kuhusu mahusiano ya kimamlaka ya ndani, kutambua wasaidizi wa kiasili, kuwezesha umakini katika majadiliano yaliyo angazia mtoto, na uvumilivu katika kuwezesha ufahamu wa jamii na hatua ya kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Njia hii ya Kukuza Utulivu ilikuwa ya makusudi kuwa pole pole na ilionyesha hatua na ubadilifu wa jamii kwa kuwahusisha watu mbalimbali katika majadiliano, kujadili masuala kwa uwazi, na kuchukua maamuzi ya pamoja. Ujuzi wa juu wa uwezeshaji uliokuwa ulihitajika katika mchakato huu haukuwepo katika mashirika mengi ya ulinzi wa watoto, kwa sababu mfumo wa kibinadamu unazingatia utaalamu wa kiufundi na hatua za haraka za kuafikiwa.

Mambo ambayo yalihujumu umiliki wa jamii ni pamoja na kuanzishwa kwa mapema kiasi kikubwa cha pesa kabla jamii kupata mwamko wa kina wa udhaifu wa watoto au kukuza fahamu ya uwajibikaji wa pamoja. Kuanzisha kwa mapema kwa pesa, kuliongoza wenyeji kujihusisha katika kazi kama njia ya kupata mapato badala ya kutimiza wajibu wa pamoja kuwalinda watoto. Sababu nyingine ilikuwa na kikwazo ni njia za wakala kujihusisha na jamii, kushindwa kuendeleza mawazo na rasilimali za mitaa, na matumizi ya mbinu ya juu-chini. Umiliki kidogo ulijitokeza wakati wakala wa nje walithibiti nguvu, walichukua maamuzi, na "kupandisha bendera yake", kwa mfano, kuweka saini na majina yao. Umiliki pia uliharibika wakati watendaji walijifanya kama "wataalam 'ambao walitumia mbinu mbadala kuelimisha wananchi kuhusu ulinzi wa watoto. Mbinu mbadala mara nyingi husababisha watu wa jamii kuona kazi hiyo na mawazo kama yanaongozwa na wakala badala wa wao wenyewe. Katika baadhi ya matukio mengine, kulikuwa na utatanishi wa kashifu mawazo ya kutoka nje-kama "haki za watoto" ambazo hazikuambatana na utamaduni wa wenyeji.

*Mtazamo Muhimu*

Ingawa umiliki wa jamii na madaraka ya umma ni muhimu, ni muhimu kwa kuuliza jamii ni nani na pia ni nani ambaye ana mamlaka ya maamuzi. Ni kawaida kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kufanya kazi na viongozi wa jamii, kufanya majadiliano ya wazi kadhaa, ambapo maamuzi hufanywa kuhusiana na kutengeneza CWCs. Mbinu hii ina tatizo kwa sababu mara nyingi kuna wale watu ambao wanabaguliwa, wakiwemo watoto na maskini wa maskini, ambao hawaendi katika mkutano kama hiyo au wanahudhuria bila kutoa sauti. Kwa sababu maamuzi mchakato si ya pamoja, si vyema kuzungumzia umiliki wa jamii. Zaidi ya hayo, watu ambao hutawala katika mikutano hiyo wanaweza kuwa ni ma chifu na jamaa zake au wanachama wengine wasomi katika hiyo jamii. Hakika, hiyo mapitio iliripoti kuwa madhara yasiyotarajiwa wakati mwingine husababishwa na uimarishaji wa miundo ya ndani yenye nguvu ambao hutenga au kubaguwa watu mbalimbali au vikundi vidogo. Masuala haya na mengine ya kimaadili yanaweza kusimamiwa kwa kudumisha msimamo muhimu na kufanya kazi kulingana na haki za kijamii ambazo zinasisitiza kwa hali ya juu ya kushirikishwa kwa watu wote kwa usawa.

Masuala ya kimaadili hutokea mara nyingi katika kazi ya ulinzi wa watoto (Graham, Powell, Taylor, Anderson, & Fitzgerald, 2013; Wessells, 2009b) na kuenea katika mapitio. Katika baadhi ya matukio, serikali au mashirika ya ulinzi ya watoto zilizowekwa na CWC kwa jamii, na pembejeo kidogo au msaada kutoka kwa watu wa ndani. Mbinu hii za kulazimishwa zilionyesha kuchanganyikiwa na chuki, na pia kudhoofisha nia ya kutumia na CWC. Wakati mwingine CWC iliundwa kuwa namna ya mifumo sambamba na yenye uhusiano chache na miundo iliyopo ya jamii na rasilimali. Kwa bahati mbaya matokeo yake yamekuwa ni ya kudhoofika au kubaguliwa kwa misaada zilizopo, ambazo zingekuwa na uwezo mkubwa wa kuwa endelevu.

**Hatua Inayoendeshwa Na Jamii: Kielelezo kutoka Sierra Leone**

Kufuatia mapitio ya kimataifa, takriban mashirika 15 yasiyo ya kiserikali, UNICEF, na wafadhili walianzisha kujifunza miongoni mwa mashirika kuhusu kituo cha Utaratibu wa Jamii. Ulinzi wa Watoto na mikakati ya Ulinzi wa Watoto. Kutaka kuendeleza na kujaribu mbinu tofauti, inayoongozwa na ulinzi wa watoto, kikao hiki kiliamua kuchunguza kama CBCPMs zinaweza kufanywa ziwe na nguvu zaidi kupitia uongozi wa jamii unavyotokana na hatua za kuimarisha uhusiano rasmi wa masuala mbali mbali ya mfumo wa ulinzi wa watoto. Tulionelea mbinu za kuanzia chini kwenda juu katika mfumo wa kuimarisha kwa sababu jamii inatoa uteuzi na kuimarisha ushirikiano na wadau rasmi. Katika kujenga viwango vya juu vya umiliki wa jamii, tulitumia utafiti wa kushiriki na kutenda (PAR) iliolenga kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. PAR ni kundi ya mbinu ambazo misingi yake inatokana na kazi ya Paulo Freire (1968) na wengine, ambazo zinahusishwa na vipengele kama vile uwezeshaji wa ndani, na haki za kijamii na zinazo sambaza taarifa hizo kwa kutumia mbinu kama hizo na shirikishi tathmini ya vijijini (Chambers, 1994).

Katika mbinu za kutumia PAR, jamii hushikilia madaraka, kwa vile wao ndio hufafanua tatizo na kisha kuchukua hatua za kibinafsi ili kushughulikia hilo jambo, kupitia msukumo wa jamii. Nitaelezea kazi yetu na matokeo ya muda mfupi nchini Sierra Leone, nikilenga kazi iliyofanywa kati ya Januari 2011 na Juni 2014, kabla ya ugonjwa Ebola kuanza.

### *Mazingira Sierra Leone*

Sierra Leone ina wakazi wengi vijijini, takriban watu milioni sita. Ni safu karibu chini (177) juu ya Ripoti ya Maendeleo kwa binadamu (UNDP, 2013) na ana wastani wa kuishi wa miaka 46-47. Katika maeneo mengi ya vijijini, watu hushiriki katika imani na desturi za jadi, kama vile desturi za mazishi na machifu na wazee wakitatua migogoro. Nchi imegawanywa katika maeneo ya machifu 144, kila mmoja ukiongozwa na chifu Mkuu.

Kuanzia mwaka wa 1991 hadi 2002, Sierra Leone ilishuhudia vita vya kikatili ambapo watoto walikuwa wahusika wakuu (Denov, 2010; McKay & Mazurana, 2004; Wessells, 2006). Kushughulikia masuala ya ulinzi wa watoto wakati na baada ya vita, mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yalianzishwa na kufunza CWC nchi nzima. Wakitaka kusaidia haki za watoto na ustawi, serikali ilipitisha Sheria ya Haki za Watoto mwaka 2007, ambayo ilipewa jukumu ya uanzishaji wa kikundi cha wanachama 13 wa CWC katika kila kijiji. Jukumu lao lilikuwa kufuatilia, kujibu, na kuzuia ukiukwaji dhidi ya watoto na kutaja ukiukaji jinai kwa mamlaka kama vile polisi. Baada ya hapo, serikali iliamua kuanzisha na kuunda CWC katika Utemi badala ngazi ya kijiji. Mashirika yasiyo ya kiserikali yalisaidia utekelezaji kwa kutoa mafunzo kwa wanachama CWC na kutoa elimu ya haki za watoto katika ngazi ya jamii. Elimu ya haki za watoto ilifanyika hasa katika hali ya, juu-chini namna ambayo wataalam shirika lisilo la kiserikali walifundisha wenyeji, dhana na lugha ya kimataifa kwa ulinzi wa watoto na madhara inayofanywa na mazoea ya kimila kama vile adhabu ya viboko.

### *Mpangilio wa utafiti*

Takwimu. 2 inaonyesha, utafiti ulihusisha kujifunza kupitia ethonologia na kisha kutumia kwa miraba miwili kwa kuchagua mbinu za kubahatisha kujaribu msukumo wa jamii wa kuingilia kati. (Stark et al., 2014). Wazo hili lilikuwa la kujifunza kwa kina kuhusu taratibu za jamii na rasilimali na kuendeleza hayo katika awamu ya utekelezaji. Katika kila moja ya wilaya mbili, kulikuwa na makundi mawili ya jamii tatu. Maeneo hayo yalikuwa mapema yameingiliwa kati na hali ya kuchelewa kuingilia kati, kwa mtiririko huo. Katika hali ya kutumia mbinu ya mchanganyiko, utafiti wenye utaratibu ulitumika kupima hatari ya watoto na matokeo bora katika msingi (T1) na katika maeneo mawili baadaye (T2 na T3). Nitajadili maelezo ya T2 kwa sababu, ugonjwa wa Ebola umefanya kuahirishwa kwa mkusanyiko wa matokeo ya T3. Habari/data stahilifi ilitoka kutoka kwa wachunguzi wanaoishi katika jamii, tafakari za vikundi kutoka kwa wanajamii, na mahojiano na watoto, watu wazima, na wahudumu wa afya.

### *Njia Mbalimbali Za Pamoja*

Kufanya utafiti huu uwe wa umuhimu zaidi, kwa kuwa kufikia ngazi za juu zaidi, na kuepuka mbinu ya utendaji zaidi, tulishirikiana sana na watendaji wa

mitaa katika awamu zote za utafiti. Kwa msaada wa UNICEF, sisi tulifanya kazi kwa karibu na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Masuala ya Watoto na Kamati ya Taifa Ulinzi wa Watoto (CP Com), ambayo ilihusisha wakilishi kutoka watendaji wa ulinzi wa watoto kama vile Save the Children, World Vision, Plan International, na Goal.

CP Com ilisaidia kutengeza utafiti huu katika mazingira ya Sierra Leone, kupeana ushauri kuhusu maadili ya utafiti, na kushirikiana katika uteuzi wa maeneo. Ili kuwawezesha kujifunza zaidi, tulilenga wilaya mbili tu. Hata hivyo, tulitaka kuingiza kabila na lugha tofauti na kufanya kazi katika maeneo yanayoangaziwa kama mfano wa mikoa husika. Kufuatia ushauri kutoka kwa wanachama CP Com, tuliamua kufanya kazi katika wilaya ya Moyamba kusini, sehemu ya watu wa kabila la Mende, na Wilaya ya Bombali kaskazini, sehemu ya watu wa kabila la Temne. Kushauriana na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ulinzi wa watoto, ndani ya kila wilaya hizo, walihusika kwa kuchangia kuchagua makundi mawili katika zile vijiji vitatu kwa kila moja. Nguzo zilikuwa zimeandana takriban (maelezo kamili yalikuwa nadra) kuhusiana na masuala ya ulinzi wa watoto, usaidizi na huduma zinazopatikana, na hali ya kiuchumi kwa jamii.

Mbinu hii ni shirikishi ambayo CP Com ilishauri na kikundi cha Columbia kutoa utaalamu wa kiufundi katika utafiti huu ilikuweka mikakati ya kuwa na sera ya kuleta mabadiliko baada ya muda. Kwa sababu CP Com walikuwa wameona umuhimu wa utafiti huu, walisaidia na walitaka kujifunza kutokana na huu utafiti.




**Takwimu. 2 Ubunifu wa hatua ya utafiti**

## *Awamu ya Ethnografia*

Madhumuni ya awamu hii ya Ethonografia/mila ilikuwa ni kuimarisha uaminifu na kujifunza kwa undani masuala kuhusu watoto, ambayo yangeweza kutoa riporti kwa jamii kwa njia ya kutafakari kwa pamoja na msukumo wa utendaji wa jamii.Watafiti wa Sierra Leon walikuwa wamepata mafunzo, waliishi na kufanya kazi katika vijiji kwa wiki kadhaa na walikuwa wakisimamiwa na washauri wenye uzoefu. Watafiti waliepuka maneno yanatumika kimataifa kama vile ulinzi wa watoto au haki za watoto, na walijaribu kunasa hadithi za wenyeji. Walijiweka kama wanafunzi, watafiti waliuliza jamii kuwafundisha kuhusu maoni yao ya watoto na kujibu maswali kama vile: Mtoto ni nani? Je, madhara makuu kwa watoto ni gani? Je, kawaida hufanyika nini wakati madhara fulani yanafanyika? Je, watu hufanya nini kwa kawaida wakati visa vya ukiukaji wa jinai kama vile ubakaji wa mtoto umetokea?

Watafiti walitumia mbinu kama vile uchunguzi wa washiriki, katika mahojiano ya kina na iliofanywa kwa mshiriki ana kwa ana, na majadiliano ya vikundi. Mahojiano na

majadiliano ya vikundi, ambazo zilifanyika katika lugha za kienyeji, kuuliza maswali yasiokuwa na jibu moja na ilikuwa rahisi kubadilisha kisha kufuata mawazo ya washiriki. Mahojiano yalirekodiwa na yalitafsiriwa kwa Kiingereza, na baadye mshauri kuchunguza usahihi wake. Mahojiano pia yalikuwa yakifanywa kwa lugha ya Kiingereza kwa wafanyakazi wa ulinzi wa watoto kama vile polisi, wafanyakazi wa serikali za kijamii, na wafanyakazi shirika lisilo la kiserikali.

Kubaini iwapo maoni ya wenyeji yalitofautiana kulingana na jinsia na umri, majadiliano ya vikundi yalihusisha makundi ya watu kumi ambao wote walikuwa wanawake, wanaume, vijana wasichana, au vijana wavulana wenye umri mdogo. Katika majadiliano hayo ya vikundi, washiriki kwanza walitambua na kutaja madhara makuu kwa watoto, na kisha kuorodhesha madhara matatu makuu na ya maana kubwa yanayowahusu watu. Kwa kila moja ya madhara iliyotambuliwa, watafiti kuchunguza na kutambua njia za kawaida za majibu na kutambua watendaji, maamuzi na hatua zilizochukuliwa, matokeo, na jinsi watu tofauti waliweza kuona matokeo.

Matokeo yalionyesha kwamba wenyeji walikuwa na maoni tofauti sana kuhusu watoto na madhara yanayo wakumba kuliko yale yaliopo katika viwango vya kimataifa (Wessells, 2011; Wessells na wenzake, 2012.). Mtoto hakutambuliwa kwa umri wake lakini kama mtu ambaye alikuwa tegemezi kwa wazazi ama mwenye hajafanya ngono. Madhara ya juu ya yote kwa watoto, yalikuwa, watoto walio nje ya shule /kuwacha shule, mimba ya ujana nje ya ndoa, kazi nzito, na uonevu wa watoto ambao hawaishi na wazazi wao waliowazaa. Madhara yaliyotajwa zaidi ni pamoja na: kupiga motto, ukatili, unyanyasaji wakingono (ikiwa ni pamoja na ubakaji na ujamiiano wakijamaa), kutelekezwa na uzazi mbaya, uchawi, utekaji nyarana kafara za ibada, na haki za watoto. Raia wa kawaida hawataji shida kama vile utahiri wa wanawake, ambao umeenea Sierra Leone (UNICEF, 2013).

Haki kwa watoto ilitajwa mara kwa mara kama madhara kwa watoto, ilitushangaza sana sisi kwa sababu haki za watoto zipo kwa kutetea na kulinda watoto (Tazama pia Behnam, 2011). Wazazi waliovujika moyo walisema kwamba haki za watoto zimedoofisha malezi hawawezi kuwadhibu kuwatandika viboko watoto ili kuwafunza madili na tabia nzuri. Hata Wafanyi kazi wa haki za watoto walikosolewa kwa kuwapa watoto majukumu madogo. Visa vilitokea kwa sabubu athari ya haki za watoto kwa zimeleta madhara. Mama mmoja alikuwa amekasirika alielezea vile hawezi kumtandika bintiye mkaidi kwa kuofia kuripotiwa kwa wafanyi kazi wa haki za binadamu, inambidi kumnyima chakula kama adhabu.

Kwa njia ile ya kuitikia kwa madhara kwa watoto, ilionyesha kuwa kuna mambo yaliotafautiana kati ya rasmi na yasio rasmi kulingana na hazima za kulinda watoto. Hata hivyo wafanyikazi wa kulinda watoto walipendekeza CWC’s wawe wa kutuliza joto, lakini hawa wananchi wa kawaida hakuna aliyemtaja au kwenda kutoa ripoti kwa CWCs. Visa vya madhara kwa watoto, zaidi ya 90% watu wa kawaida walipendeza ni bora kusuluhisha kwa kuenda kwa chifu au wazee wa jamii yao. Kwa mfano msichana akipata mimba, wazazi wake huambatana kwa familia ya mkosaji na kufanya mazungumzo, hatimaye familia ya mkosaji inakubali kumsaidia msichana katika kipindi cha uja uzito wake, kulipa fidia ya wakati amepoteza akiwa nje ya shule, na kumlazimisha mvulana kumuoa msichana. Wakati mwingi wasichana huwa hawafurahi na uamuzi huo, ingawaje familia huwa ina linda msichana na pia jina la familia. Hata kwa visa

vya ubakaji wananchi wa kawaida walisema kuwa watu wengi hawataki kuripoti kisa cha uhalifu kwa polisi sababu ni; wako mbali na ofisi, hawana nafasi wanaendelea na kazi za shamba, kuhofia kwamba hakuna hatua itachukuliwa. Kwa sababu ya mila, watu wanachukulia kijiji chao kuwa kama watu familia moja hivyo hakuna kuzungumzia mambo yao na watu wa nje.

Matokeo haya na mengine (Thompstone 2010) yanaonyesha kwamba CRA haifanyi kazi na watu wanapendelea sana kutumia njia zisizo rasmi za kulinda kuliko zile rasmi.Walitoa onyo kuhusu kuhusika kwa juu-chini kwa CWCs kutomiliki jamii na kuwa hawana ufahamu wa kutosha kutia jamii nguvu.Walisistitiza umuhimu wa njia mwafaka za kuwasilisha haki za watoto. La muhimu zaidi ni kuwezesha njia za kuhusisha jamii na kushiriki katika mifumo rasmi ya haki za watoto.

*Njia ya Mpango*

Washauri walielezea matokeo ya awamu za mila kwa alaiki ya watu kijijini and kuwauliza kama matokeo hayo yalikuwa sawa. Watu walikubaliana na kuwashukuru kwa kuwaregeshea matokeo.Kuwa na picha ya ujumla wa madhara kwa watoto watu walifikiria nini wao watafanya.Hii ilikuwa fursa ya maana kuwezesha kwa pamoja kimawazo na umilikaji wa ujamii.

Njia ya mpango kwa jamii ilirahisishwa kwa kuanza kwa kasi, njia za kitaalum na kuwatuza wao kwa sababu wao sio wafanyakazi wa kulinda watoto. Kuanzisha njia za mpango wa kuwaezesha na umuhimu wa kushirikisha wasichana na wavulana. Wa Sierra Leone wawili waliajiriwa na kufunzwa, moja kutoka Moyamba na wengine Bombali- waliweza kuzungumza lugha ya wenyeji vizuri na kuelewa mazingira na kanuni za jamii. Walifunzwa jinsi ya kuuliza maswali yasiokuwa na jibu moja, kuwezesha kikundi kujua umuhimu wa jambo. Kuuliza maswali zaidi na kutaja mambo wanaodhania, hivyo kuwezesha njia murwa za kusuluhisha shida hizo. Baadaye wafanyi kazi na washauri wakuu, watafiti wa kimataifa na msimamizi mkuu, waliiishi siku kadha kwa kila kijiji na hatimaye kuenda kwa vijiji vingine.

Jambo la kwanza ilikuwa jamii kuchagua ni madhara gani kwa watoto wanafaa kushugulikia. Kwa kazi hii na ya baadaye, njia hiyo ilikuwa ya muhimu ya kutoa uamuzi na matokeo yaliopatikana. Washauri kwanza walizungumza na machifu na kuwaelezea umuhimu wa kumiliki jamii, ili kuwaepuka chifu na wenye mamlaka kutawala mpango huo. Chifu wa Kuu walikubali kutoelekeza mpango huo na ila kuhimiza ofisi yake kuheshimiwa kwa kupata repoti na mawasiliano mara kwa mara. Msimamizi aliuliza mpangilio wa maswali ili kuwawezesha kufikiri vile wataweza kuwahusisha wana jamii wote kwa mipango. Mazungumzo yalifwatiliza taratibu zifuatazo hapo chini:

| | |
|---|---|
| Msimamizi: | Ni vipi jamii yote inaweza kuchagua ni madhara gani kwa watoto ya kushugulikia |
| Mshiriki: | Tunafaa sote kuwa na mkutano kwa baraza ya chifu. |
| Msimamizi: | ”Je, watu wote wanashiriki kwa baraza ya chifu?” |
| Mshiriki: | Ndio kila moja hudhuria |
| Msimamizi: | ”Nimepatana na msichana kipofu hapa. Je yeye hudhuria baraza? |

| | |
|---|---|
| Mshiriki: | "Hapana. Hawezi kufika kwa baraza" |
| Msimamizi: | "Je kuna watu kwa kijiji masikini sana kuliko wengine?" |
| Mshirki: | "Ndio. Kunao masikini sana hata wawezi kuwalisha familia zao" |
| Msimamizi: | "Je wale masikini fukara huja mikutano ya baraza?" |
| Mshirki: | "Hapana. Wanafanya kazi wakati mwingi, kwa hivyo hawana nafasi" |
| Msimamizi: | "Je, wasichana na wavulana wanahudhuria mikutano ya baraza?" |
| Mshiriki: | "Ndio, na wanfurahia kuwa hapo" |
| Msimamizi: | " Je, msichana wa wastani, wa miaka 10, anaweza kuongea kwa baraza?" |
| Mshiriki: | "Labda la. Ni kwa sababu ya heshima kwa wazazi wake na wazee." |

Mazungumzo na watu wengi kwa vikundi na mmoja kwa mmoja, iliwezesha jamii kutambua njia tatu ya mipango. Kwanza ni vikundi vya watu wazima na watoto wakipanga pamoja na kuwatembelea manyumbani wale wasioweza kufika kwa baraza. Pili, mazungumzo ya vikundi vidogo vya vijana wasichana, vijana wavulana, wanawake, wanaume na wazee, hii inawezesha washiriki kuzungumzia mambo ya kindani bila wasiwasi.Tatu, kuendeleza mazungumzo ya baraza mara kwa mara na kupata majibu ya utekelezaji kutoka kwa vikundi vidogo vya mazungumzo. Mpango huu unawapitia wengi sauti, kujulikana na jamii na kuitumia kufanya uamuzi wowote kuhusu jamii kuliko hapo mbeleni.

Kusimamia mipango katika kila sehemu ya vijiji vitatu, na jamii kuunda kikosi maalum kwa kila kijiji.Kila kijiji kilichagua wanachama watano, moja kutoka kwa kila kikundi kidogo. Ili kusaidia kwa njia za mipango, chifu mkuu alichukuwa wadhifa wa kuwa kinara, kusimamia mambo ya kijiji, kusikiza na kutia moyo mazungumzo ya kikosi maalum na kutoa repoti. Kwa kupata mapendekezo kutoka kwa kila jamii, kikosi maalum kimekusanya mapendekezo ambazo yalizungumziwa na jamii wakitumia zile njia tatu zimetajwa hapo juu.

Labda kuingilia kati kwa mambo ambayo yanawezekana na ushirika wa serikali inabidi kupanga mipango wakati huo huo wakizingiatia kuipa kuingilia kati kipaumbele, Kwa kuwa waangalifu kwa sababu ya hadi za uongo, wenyeji walichagua hoja moja ambao serikali ingetekeleza.

Baada ya mazungumzo ya kina, hoja ya mimba kwa vijana ilichaguliwa na kupewa kipa umbele ili kutekelezwa, na jamii kutoka zile wilaya mbili. Hoja hili la mimba kwa vijana ambalo lilikuwa inaleta hisia mbaya (Coinco, 2010; Wessells, 2011) kusababisha watoto kuacha shule na kuwafanya wazazi wachanga kujihusisha kujiuza kingono ili wapate riziki. Kutumia njia za kitamaduni kuweka sheria, kushindwa kukomesha mimba kati ya vijana. Baadhi ya watu katika jamii walikuwa wamesikia kuhusu kazi ya Marie Stopes na walitaka jamii yao kufaaidika na mambo kama mpango wa uzazi, Elimu ya afya ya uzazi na ngono na kupata ujuzi wa maisha.Mazungumzo kati ya Washauri na Madaktari kutoka wilaya ilionyesha ya kwamba serikali iko tayari kusaidia na njia za mpango wa uzazi kama kondomu, njia ya kupandikiza vidonge vya dawa mkononi, na kuwafunza wauguzi jinsi ya kuvipandikiza vizuri. Kuchagua hoja

ya mimba kwa vijana kulitoa mfuko wa wasiwasi kwa taifa na kuifanya iwajibike. Tatizo hili ilisambaa kote na umuhimu ni kwamba Raisi wa Sierra Leone alitangaza hali ya hatari, na kuwahimiza wananchi wote kusaidiana kuzuia mimba za vijana.

Ushawishi wa kuingilia kati kwa mipango, jamii iliamua kuongezea viongozi ambao ni vijana kama wanchama wa kikosi maalum. Kwa kuongeza vijana kwa kikosi maalum, iliwapatia sauti na uwezo kuwashawishi na kutambua kwamba ikiwa mimba za vijana zitapungua basi vijana wavulana na vijana wasichana watahitajika kuwa mstari wa mbele kubadilisha kanuni za jamii.

Kufuatia mazungumzo baina Marie Stopes na Restless Development (shirika lisilo la kiserikali - Uingereza), Kikosi maalum cha Utekelezaji kilitambua vitendo ambavyo vilitakikana kuwa kati ya zile madokezo za awali za kuingilia kati. Kuhusu mpango wa uzazi , walipanga mafunzo kwa jamii na mazungumzo ya kubalehe, chanzo cha mimba, thamini ya mpango wa uzazi na uamuzi wa vijana kutumia njia za mpango wa uzazi na kuchelewesha kufanya ngono. Kuhusu afya ya uzazi na ngono, walipanga jamaa kufunzwa njia za mpango wa uzazi, jinsi ya kujizuia na magonjwa ya zinaa, kuelezea shauku ziliopo kuwa njia za mpango wa uzazi zinaweza fanya mtu asiweze kupata watoto na vile kutunza mimba inapotokea. Kuhusu kupata ujuzi, walipanga vijana wadogo na wa makamo kuwa mfano mwema kwa jamii. Hasa walitaka vijana wasichana kuweza "kukataa" ngono wasiotarajia, kutongozwa na wanaume wanaoshikilia nadhifa kubwa , kuzungumzia na kujadiliana kuhusu tabia za ngono na rika zao, kuepuka na desturi za wasichana na wavulana kulewa pombe na kufanya ngono bila kinga hapo kwa hapo. Kwa kawaida vijana wavulana na wasichana, watu wazima wanawajibu wa kutekeleza, kusaidiana kubadili kanuni za jamii kwa kupata matokea bora.

Katika kila jamii walichagua vijana watano wasichana kwa wavulana kuwa waelimishaji marika, walifanya kazi pamoja na wanachama wa Kikosi maalum, vikundi vidogo tafauti ile kutekeleza. Shirika lisilo la kiserikali lilitoa mafundisho ya msingi kwa waelimisha rika na kuchangamsha fikra zao kuhusu jumbe muhimu za kusambazwa katika warsa ya wiki moja. Mafunzo ya kwanza ilikuwa kati ya June-July 2013 na mafunzo ya kufuatiliza ikiwa March 2014. Kufuatia mafunzo ya kwanza kwa maelimishaji rika, serikali iliwafunza wauguzi wazamili na ndipo mpango wa kuingilia kati ulianzishwa. Licha na haya kulikuwa na shida iliyokusudiwa katika mipango ya kupanga na kuteleza, mazungumzo yalichangia ongezeko wa ufahamu na kuhamasisha wanaounga mkono mpango wa kuingilia kati.

*Msukumo wa Jamii*

Kuingilia Kati. Njia ya kuingilia kati ilimetoa hati kuhusu Wasimamizi wa Sierra Leone kufanya kazi kamaViranja, wakitumia njia za kutazama washiriki ili kunakili mambo kadha wa kadha. Baada ya kuingilia kati kuanza June 2013,

alitumia muda wa 75% wakifuatilia.

Jedwali. 2 inaonyesha madokezo 10 muhimu ya njia za kuingilia kati ambazo zimetokea kwa muda. Katikati ya mipango kulikuwa mazungumzo ya pamoja na uaamuzi wa pamoja. Wakati wote wa kutekeleza, wanachama wa kikosi maalum au wanavijiji wenye mamlaka waliandaa mazungumzo barazani, wakizungumzia kubalehe, njia za mpango wa uzazi, magonjwa ya zinaa, umuhimu wa kucheleweshа kufanya ngono au kufanya ngono iliyo salama. Waelimisha rika pamoja na wanachama wa kikosi maalum, walitembelea watu manyumbani kupata maoni ya familia na watoto yaliotengwa. Mazungumzo mengi yalifanyika kwa kufuatizia vijana wakicheza michezo za kuigiza, kuimba, wakila, wakiwa shuleni na wakati wanafanya mambo yao ya kila siku.Mazungumzo yaliofanyika nje na ndani ya baraza yalilenga jamii kubadilika. Hapo mbeleni wazee walikataa utumiaji wa njia za mpango wa uzazi, waliofia itapotosha wasichana. Hata hivyo kwa muda, kina mama waliweza kuwashawishi wanaume wao kwamba binti zao watumie njia za mpango wa uzazi kwa sababu wanashika mimba.

**Jedwali. 2**

Madokezo Kumi muhimu ya msukumo wajamii kuingilia kati

| Madokezo | Maelezo |
|---|---|
| Mazungumzo ya pamoja, kujitambua na kujadiliana | Mawazo na mazungumzo ya pamoja yanaendelea na kutokea barazani na kwa vikundi vidogo kati ya vijana wasichana, vijana wavulana, wanaume wazima na wazee. Kuhusu ni jambo gani litapewa kipaumbele, na ni vipi litasuluhishwa na mambo mbalimbali kuhusu mimba ya vijana. Mazungumzo haya yaliibua mawazo ya pamoja na mawazo tafauti yakujadiliana na kujiandaa tayari kupokea ujumbe kuhusu mimba ya vijana. |
| Uamuzi wa pamoja, kuezesha na jukumu | Jamii wenye waliamua ni jambo lipi la kusuluhishwa, vile kuisuluhisha, ni nani atawakilisha katika kikosi maalum kijijini na kwa mambo mengine. Kutambua uamuzi na mipango ya kuingilia kati kuwa ni wao, na hivyo kuchukua jukumu la kufanikisha. Waliwezesha kuwahimiza kila mtu kushiriki, kuhamasisha vikundi tofauti vidogo, kuanzisha shugulisha na vitendo hivyo kuongeza idadi ya watu. |
| Unganisha jamii na huduma za afya | Ofisi ya Daktari wa Wilaya, ilitoa dawa tofauti za mpango wa uzazi na kuwafunza wauguzi mzamili kupandikiza vidonge vya dawa. Mashinani, walianzisha usiano wa kusaidiana kati ya mwenyeji na waguzi waliofunzwa njia za mpango wa uzazi. Watu walitembelea hospitali baada ya kuanzisha mpango wa uzazi. Wauguzi walialikwa tembelea vijijini na kusaidia kuelimisha kuhusu kubalehe, ngono, afya ya uzazi na uja uzito |

| | |
|---|---|
| Elimu ya marika | Waelimishaji rika waliochaguliwa na jamii waliwafunza rika zao na watu wazima kuhusu mambo ya mpango wa uzazi, afya ya uzazi na ngono na ujuzi wa kimaisha.Pia uelimishaji rika ulionekana kupitia mazungumzo kati ya wazazi, wanawake na wanaume na kadhalika |
| Utumiaji wa Utamaduni kama vyombo vya habari | Waelimishaji rika na wengine waliandaa shuguli za kuelimisha za kitamaduni kama nyimbo na mchezo za kuigiza. Baadaye vijana na watu wazima walizungumzia ukweli ulioko ndani ya nyimbo na mchezo za kuigiza, kujadiliana kuhusu hatari, kukubaliana na faida ambazo zipo kati ya vijana wanapofanya uamuzi bora maishani, |
| Kiongozi Kijana na jumbe | Vijana wavulana na wasichana walikuwa washuhuri kwa utendaji, utekelezaji wa mpango wa kuingilia kati. Walitunga jumbe na kuzisambaza kuathiri watu wengine wa makamo. |
| Kuleta pamoja na kupeleka huduma kwa kijiji | Wakilishi wa vikundi tofauti vidogo(vijana wasichana, vijana wavulana, wanawake wazima, wanaume wazima na wazee) walihusika katika kikosi maalum kwa msukumo kwa jamii kuhusu kuzuia mimba kwa vijana. Kutembelea manyumba kulileta sauti na maoni ya waliotengwa kama watoto walioacha shule na walio na ulemavu |
| Uamuzi wa mzazi-mtoto | Wazazi na watoto wao walianza kuzungumzia kuhusu kubalehe, afya ya uzazi, ngono na kuzuia mimba kwa vijana. Wakati mwingine watoto waliweza kuwakosoa wazazi wao kwa kuelewa vibaya. |
| Wajibu wa Ushari | Kwa kushugulika kwa vitendo kama mchezo wa kuigiza na nyimbo, vijana wakiawamo wavulana walionyesha ishara kwamba walitaka kuzuia mimba kwa vijana. Wazee na wazazi walitoa mfano bora kwa kujitolea kupunguza mimba kwa vijana. |
| Mamlaka ya Halali | Machifu wakuu walionyesha wazi kuunga mkono kuzuia mimba kwa vijana na kuwasihi watu kushirikiana kwa kuingilia kati. Viongozi wengine kama waalimu na viongozi wa makanisa pia waliunga mkono kuzuia na kupunguza mimba kwa vijana. |

Kwa kila dokezi, msukumo wa jamii kwa mpango wa kuingilia kati, waliamua lini, wapi na ni vipi kutekeleza mpango wa kuingilia kati. Kikosi maalum kilifanikiza mpango huu, hata hivyo uamuzi ulikuwa umefikwa na vikundi vidogo vya jamii.Utekelezaji ulifwatilizwa na mpango kutoka kwa jamii, haikufuata mkataba wowote lakini ulikuwa umetungwa kwa hali ya juu kuvutia shirika, vijana na watu wengine. Njia hii ambao ina uwezo wa

kubadilisha, iliwezesha mpango wa kuteleza kwa kubunia nafasi mpya, changamoto zilizotokea kwa sababu ya ongezeko ya jamii kuwa macho au kupinzana. Kufuatia njia za kanuni za jamii, wenyeji waliendeleza mpango na kuamua ni shuguli zipi zinazohitajika na jinsi ya kuzitekeleza.

Wakati wote wa mpango wa kuiguilia kati, wakiwa macho na kutambua kuhusu njia tofauti wa mpango wa uzazi, ngono, afya ya uzazi na ujuzi wa maishani, ilitangazwa kupitia jumbe za msukumo wa vijana na utumiaji wa vyombo vya habari wa kitamaduni. Waelimishaji rika ambao walikuwa viongozi wa vikundi vya vijana, walifanya shuguli kama nyimbo na michezo ya kuigiza (muhtasari wa tabia ya mtu) iliyoingiliana na mila za wenyeji, yenye msukumo wa kusisimua. Katika shuguli moja wasichana na wavulana waliwalika jamaa kuigiza mchezo sehemu ya Pili. Sehemu ya Kwanza msichana na mvulana walienda kwa chumba cha video, wakalewa na kuvuta sigara na kisha kufanya ngono bila kinga. Msichana alishika mimba hivyo yeye na mvulana wakaacha shule na "kupoteza maisha yao ya baadaye" Sehemu ya Pili inaonyesha msichana ule ule na mvulana wakizungumzia mawazo yao ya "kupata elimu" na nini watafanya kutimiza lengo lao. Mchezo huo wa kuigiza ulichangamsha mazungumzo kati ya wanajamii, wakigusia shida za mimba kwa vijana na faida katika sehemu ya pili kwa watu binafsi, familia na jamii.

Uongozi wa watoto na jumbe za maana kwa mpango wa kuingilia kati ni sababu vijana wanajua vizuri jinsi ya kuwasiliana na kuwavutia vijana wengine. Kule Moyamba vijana walitengeneza ujumbe "5920" inayo maanisha dakika tano za raha, miezi tisa za uja uzito, ikifuatiwa na miaka miwili yakuwa nje ya shule, na mwishowe hauna chochote, kwa sababu wamepoteza elimu yao. Vijana wanatumia jumbe hizi kwa mikutano midogo au mikutano mikubwa na kusisimuwa furaha na kicheko ingawaje maana yake inafaa kuwa haina utani. Vijana kutoa jumbe hizi, waliungua mkono na watu wazima, walishirikiana kwa uongozi wa pamoja na kuzidi kuwaona kuwa na maadili mazuri na kufanya uamuzi mzuri.

Wakati wa vipindi vya mipango, waze walisema kabla ya vita, wazazi walikuwa tayari wameongea na watoto wao kuhusu kubalehe, ngono na mimba na hayo mazungumzo yalifaidi watoto na familia. Ili kuwakubusha kuhusu destuti hizi, kulikuwa mazungumzo ya wazi barazani na mafundisho kutoka kwa shirka lisilo la kiserikali likihimiza mazungumzo ya mzazi na mtoto na kuleta maafikiano ya elimu na usadizi. Kwa masuala mengine, wazazi waliongoza kwa kuwasaidia vijana wadogo kuelewa mabadiliko katika mwili wao, walielezea vile wasichana wanapata mimba na umuhimu wa kuzuia mimba kwa vijana. Watoto walianza mazungumzo na wazazi na kisha kuwa walimu wakukosoa uvumi uliopo, kwamba kondomu haifai kutumiwa kwa sababu inatoka na kukwamaa ndani ya uke wa mwanamke.

Mjimu wa kuonyesha mtindo, ni njia ya kuongezea motisha kwa pamoja ili kushiriki na kufundisha miuundo mipya ya jamii kuingiliana ya kusaidiana kuzuia mimba kwa vijana. Kujifunza kwa kutazama huenda kukachangia watu kushiriki kwa mipango ya kuingilia kati. Vile watoto wanaimba na kucheza

michezo ya kuigiza, hawakutoa maelezo tu mbali walikuwa wajimu wa mtindo, kwa kuwahimiza watoto wengine kuendelea na shule, na kujizuia na shinikizo la wavulana pamoja na kuzuia mimba ya mapema. Watu wazimu walitoa mfano, kuwa wajimu wa mtindo kwa kushauri jinsi ya kuepuka mimba kwa vijana. Sauti ya kusaidia kutoka kwa Chifu mkuu na Vinara wa Chiefdom ilisaidia kuhalalisha mpango wa kuingilia kati na kuwahimiza jamii kuhusika. Usaidizi kutoka kwa wafanyi kazi wa serikali wa Idara ya Afya huenda wakachangia kwa jamii kuendelea kushugulisha na kujihusisha.

**Matokeo ya mwanzo.**

Matokeo ya mwanzo yalikuwa ni tokeo la kujenja kuhusu kulinda watoto, mipango kwa jamii na kuimarisha mifumo.

*Umiliki wa jamii*. Umiliki wa juu kwa jamii ulionekana wakati wote wa vipindi vya kupanga na kutekeleza. Wanajamii na machifu wakati mwingi walitaja mipango wa kuingilia kati kama “yetu” na kusema kwamba Mashirika yasio ya kiserekali na serikali wanawasaidia lakini hawaoungozi kwa kuingilia kati. Mara nyingi watu wamejitolea kwa juhudi na wakati wao bila kulipwa pesa au kupewa ridhaa. Kwa muda watu wengine mbali na kikosi maalum na waelimishaji rika, walishiriki na kuchangia kupanga shuguli za kuingilia kati. Hivyo mpango wa kuingilia kati ni kazi ya pamoja kwa jamii.

*Uhusiano usio rasmi/rasmi na Kushirikiana*. Mipango ya kuingilia kati ilimarisha unganisho la kushirikiana kwa jamii na vituo vya afya vijijini. Wafanyi kazi wa afya na wananchi wa kawaida wote waliripoti kwamba hapo mbeleni kabla ya mpango wa kuingilia kati, vijana kati ya umri wa 13-19 na wanajamii wengine, ilikuwa ni nadra kwao kutembelea vituo vya afya na hivyo wauguzi wakaalikwa kwenda vijijini. Mpango wa kuingilia kati hata hivyo ulibandilisha hali. Vijana wengi na wazazi wao au wazazi wao walitembelea vituo vya afya mara kwa mara kwa njia za mpango wa uzazi au kwa maelezo. Kila wakati huko vijijini waliwalika wauguzi na wafanyi kazi wengine wa afya kuwafunza wanavijiji mambo kuhusu kubalehe, mimba, afya ya uzazi na ngono na jinsi ya kuzuia mimba kwa vijana.

*Uzai wa Mpango*. Madaktari wa wilaya walitimiza ahadi zao ya kutoa njia za mpango wa uzazi na kuwafundisha wafanyi kazi wa afya. Mfanyi kazi wa kituo cha afya alijivunia na kusema jinsi vile mpango wa kuingilia kati umeongezea mahitaji ya mpango wa uzazi hasa vidonge vya kupandikwa kwa wasichana. Ongezeko la kipekee kwa njia za mpango wa uzazi ulitokea pia kwa vijiji vilivyokuwa vikilinganishwa, na makusudio ya matokeo kutoka kwa Raisi, ya kumaliza mimba kwa vijana. Ijapo kondomu za wanaume zilisambazwa kwa wingi, utafiti ulionyesha kwamba idadi ndogo ya wanaume walikuwa tayari kutumia kondomu kila wakati. Bado kulikuwa na ishara za mabadiliko. Katika

ile hali ya kulinganisha, vijana umri kutoka miaka 13-19 walio ndani ya mpango wa kuingilia kati, iliripotiwa kuwa na ongezeko ya matumizi wa kondomu ya kila wakati na kuwauliza wenzio kutumia kondomu bila kusita. Hizi ni tangulizi, tunatumai kuona mabadiliko makubwa kwa tabia na kanuni za jamii zinahusika na ngono.

*Ujuzi wa Maisha*. Wasichana wa umri wa 13-19 waliripoti kwamba kwa sababu ya mapango wa kuingilia kati, waliweza kusema "La" mara kwa mara kwa ngono isiyo hitajika. Wote wasichana kwa wavulana walisema jinsi wamejifunza kuzungumza na kujadiliana na wenzio kuhusu ngono, na vile wanaweza kupanga shuguli zao za ngono wakiangalia nguzo za maisha. Kwa kuongezea, wavulana walizungumza waziwazi kwamba wako na jukumu la kuzuia mimba ya mapema kwa vijana. Jukumu hilo lilitafautiana sana na tabia zao za hapo mbeleni.

*Mimba kwa Vijana kati ya umri (13-19)*. Utafiti kwa kuwatazama washiriki na kuwahoji wafanyi kazi wa kituo cha afya, viranja, vijana (13-19) na wazazi, ulionyesha kupungua sana kwa mimba ya mapema kwa vijana. Katika mpango wa kuingilia kati, jamii kutoka kwa wilaya hizo mbili, washiriki waliripoti kwa wastani mpango wa kuingilia kati wa kwanza kwa shule mwezi wa (September-June), kulikuwa na mimba ya mapema kwa vijana tano au sita. Tafauti na mwaka wa shule wa 2013-2014 mimba za mapema chache za vijana zilitokea. Wakati huo nusu ya jamii waliripoti kwamba hakuna kisa kipya cha mimba ya mapema kwa vijana. Nyanya ambao ni watu wanaheshimika katika jamii, walihakikisha ya kwamba ni vigumu kuficha mimba kijijini. Wote nyanya na wafanyi kazi wa kituo cha afya waliripoti, wakati wa mpango wa kuingilia kati hakukuwa na ongezeko la visa vya kuavia mimba. Matokeo haya ya kutia moyo, bado yalihitajika kupimwa na data iliyopatikana kwa njia zingine.

*Faida ya Ziada*. Msukumo wa jamii ulikuwa na athari nyingi ya faida za ziada. Washirki walisema kwamba visa vya vijana kuacha shule vimepunguwa, labda ni kwa sababu ya kupungua kwa mimba ya mapema kwa vijana, na mazungumzo mengi kuhusu "Kuweka ndoto yako" ya kupata elimu, au zote mbili pamoja. Hata katika vijiji vingine, walianza wao wenye kuzungumzia shida za ndoa za mapema. Hii ilileta mabadiliko ya uhusiano wa awamu za mila (ethnografia) ambao watu waliangazia shida ya mimba za mapema kwa vijana nje ya ndoa, na kuwa mimba kwa vijana ndani ya ndoa haikuwa na shida yoyote. Kuwa na mafunzo kuhusu athari mbaya za mimba ya vijana, wanakijiji waliuliza maswali ya kufaa kuhusu mimba yoyote kwa vijana na ndoa ya mapema. Tathimini za baadaye zitaangalia kama mabadiliko ni dalili za kubadilika pakubwa kwa wasichana na wanawake wachanga, kwa kanuni za jamii ambao walithamini kuolewa na kupata watoto mapema kwa umri mdogo.

*Mapungufu*

Uwezo wetu wakujumuisha matokeo haya una kikomo au mpaka, kwa sababu utafiti haukuhusisha sampuli ya wakilishi wa taifa ama idadi kubwa ya sehemu ya utafiti. Matokeo yaliowasilishwa hapa juu ni bora kuligana na matokeo ya awali, kwa sababu utafiti wa mwisho wa kukusanya data ulihahirishwa kutokana na hali ya hatari wa Ugonjwa wa Ebola. Pia njia ya mpango wa kuingilia kati "risasi ya fadha" Mazungumzo ya vikundi yakiendelea katika sehemu zilizokuwa na vurugu za siasa, walionekana kama vikundi vimekusanyika kutoa vurugu. Zaidi ya hayo ofisi ya dharura ya binadamu iliagiza wito wa haraka wa kulinda watoto bali na mazungumzo ya polepole ya mwongozo wa kuingilia kati. Katika mazingira ya mjini, umati wa watu uliweza kubadilika na kuwa na ushirikiano mdogo wa jamii na kukosa utambuzi wa jamii.

Hii njia ya mpango wa kuingilia kati inaweza kuwa sio chaguo la kubadilisha athari mbaya zote za kanuni na madili ya jamii. Kwa utafiti huu, watu hawakutambua kamwe kutahiri kwa wanawake kuwa na madhara kwa watoto au kuwa shida la kutatuliwa. Kwa bahati, njia za miongozo ya ndani za kubadilisha desturi mbaya zilioko nchi kama Sudan na Uhabeshi (Ethiopia). (Ahmed, Al Hebshi, & Nylund, 2009; Dagne, 2009). Ni muhimu kutimiza njia ya msukumo wa jamii, ambayo nimewasilisha kazi ya mabadiliko za jamii kuagamiza desturi mbaya kama kutahiri kwa wanawake. Jinsi vile ya kuunganisha njia hizi vizuri, ni swala muhimu kwa utafiti wa siku za usoni.

## Kuhusisha Mazoea na Sera

Utafiti wa vitendo unahusisha mambo ya thamana kwa Waweledi. Uongozi wa polepole, wa uvumilivu na wa kusingizia kitendo cha msukumo wa jamii kwa niaba ya watoto, na kutimiza viwango vya juu vya umilikiaji wa jamii kuliko kumiliki kwa njia za msukomo wa wataalam. Matokeo ya hapo awali yanapendekeza kwamba njia ya msukomo wa jamii ni ya kufaa, kwa kusaidia kuleta matokeo mazuri kwa watoto. Utafiti huu unathibitisha nguvu na matumizi ya njia ya chini-juu ili kuwezesha sera kuimarika. Kupitia msukomo wa jamii, jamii imekuza na kujitolea pakubwa kuhusika na kujifunza kutoka kwa wafanyi kazi rasmi wa afya, na kutumia huduma rasmi kusuluhisha mimba kwa vijana.

Kwa upana, njia hii iko sawa na ya busara kwa kuendeleza desturi iliyo ya kisasa. Baada ya yote, waweledi wenye ujuzi wa kulinda watoto walipatia kipaumbele kuhamasisha jamii na kuwahimiza kutia bidii kwa kusaidia na kujihusisha kulinda watoto. Kwa hali yoyote, tofauti zenye manufaa pia zipo, kwanza njia hii ina husisha kusikiliza kindani bila toa uamuzi kwa watu tofauti kuliko vile inafanyika. Pili, hii njia wa msukomo wa jamii ina hitaji walinda watoto kubadili `wajibu wao wa kuwa watalaam na kuwa wasaidizi ambao ni wanafunzi. Walinda watoto wa kutoka nje waliingia kwa jamii kama watalaam,

ufahamu na desturi za jamii huwa zinatengwa na hivyo jamii uteleza, na kwa uzoefu hao huwa wafadhiliwa. Njia iliyo rahisishwa ina sisitiza hapo juu kwamba umuhimu wa jamii ni wao kuwa wahushika, ijapokuwa wakipewa na fursa nzuri, nafasi watatiana moyo na motisa kuwa na mawazo ya pamoja ya kuchukua jukumu ya kupunguza madhara kwa watoto. Tatu, njia hii inahitaji mwendo wa polepole ili kuwezesha viwango vya juu kushiriki kwa kufanya uamuzi na kazi ya kuingilia kati, wakihusisha waliotengwa, na mpango wa pamoja ambao unahusisha vikundi vidogo tofauti. Wafanyi kazi wa shirika lisilo la kiserikali waliuza itakuaje kutumia njia ya mwendo wa polepole ilhali wafadhili na ofisi kuu ya agenti wahitaji matokeo kwa haraka. Mikakati ya manufaa kwa hili jambo nikupata fedha kwa njia mbali mbali, pamoja kuwa na mwaka, kuwa elimisha wafadhili wakitumia data iliyo asiliswa hapo juu. Kujadiliana nao ili kutimia asilimia ya sehemu ya fedha kufanyia utafiti wa majaribio kuhusu msukomo wa jamii kwa sehemu zilizochaguliwa. Pia, kuna manufaa kutambua umakinifu na msimamo wako mwenye ambao ina sisitiza ufahamu wa chanzo cha madhara kwa kutumia njia za juu-chini na njia ya haraka kupinduakia.

Maana ya ushirikishaji wa watoto katika maamuzi ya kijamii na utendaji inadhaminia umakini maalum. Vitendo ambavyo vinahitaji kusikizwa kwa njia ya kipekee. Mara nyingi, Shirika lisilo la kiserikali uwezesha watoto kushiriki wakiwa kwa ujana wao, kama vilabu vya watoto, vikundi vya vijana.Ingawa ni thamani, juhudi hizi haziwezi kuwezesha sauti za watoto kufanya uamuzi kwa jamii au kuwahusisha kabisa watoto walio na changamoto amabao hawahusiki kamwe katika mikutano ya watoto. Kuwa na mwongozo mzuri wa kupunguza shida, jamii inapanga upya mlolongo wa mipango kuwafikia watoto walio na changamoto, na kufanya agenti ya watoto kuwa uwezo wa kusaidia, kuongoza, msukumo wa jamii uliyo fahamishwa kwa niaba ya watoto.

Tukiheshimu sera, utafiti huu inasisitiza umuhimu wa kusaidia kumiliki jamii, na juhudi za msukumo kama nafasi ya kuimarisha mifumo ya kulinda watoto. Kwa bahati, Serikali ya Sierra Leone, na usaidizi wa UNICEF, na wanachama wa CP Com, ilivutia na matokeo haya. Matokeo ya ethnografia pamoja na zile utafiti zingine kama mfano (Thompstone, 2010) imetengeneza msingi kwa mtoto mgeni na sera za ustawi wa familia ambayo ina upungu wa "kuongezea muundo" kuelewa kwa kuimarisha mfumo na kwa kulenga kusaidia familia na msukomo wa jamii kwa niaba ya watoto. Pia UNICEF ilikuwa na kikundi cha kufanyi kazi wa maagenti, ambao wamekuwa wakishughulika kwa karibu na huu utafiti, kwa kuongoza kupunguza njia ya msukumo wa jamii uliyo elezewa hapo juu. Hapo mwanzo kazi ilikuwa isambazwe kote wilayani Moyamba na Bombali ikingojea kufanikiwa, na itaasilishwa katika wilaya zingine nchini. Njia ya kusuluhisha na kusambaza mawazo kote kwa jamii na Chiefdoms, itakuwa muhimu kwa mpango huu, na hekima ya kujifunza pamoja na wenyeji ikiendelea.

**Tamati**

Mara kwa mara walinda watoto walieleza kuvunjwa moyo na licha ya juhudi za kusaidia kuanzisha CWC's, kufunza wanachama wa CWC, na kuelimisha wenyeji jinsi ya kulinda watoto kulingana na sheria za taifa na viwango vya kimataifa, wenyeji hawatendi vile walivyo elimishwa, na kutumikia desturi zisizo rasmi ambazo hazina mfungamano mzuri na mfumo rasmi. Ni dhahiri kabisa njia ya nguvu ya kuimarisha CBCPM's haifanyi kazi kama ilivyotarajiwa.

Kile kinahitajika ni njia mpya ya kuimarisha CBCPM na kuwezesha ushirikiano wao wa kuwa na mfungamano wa mwelekeo rasmi kwa mfumo wa kulinda watoto. Utafili wa utendaji wa Sierra Leone unawakilisha njia mpya ya utendaji msukomo wa jamii, na kuwapatia watoto na vijana wadogo jukumu la sura ya maagenti wa mabadiliko. Jamii wenye waliendeleza mpango ya kuungana na washika madau rasmi, wenyeji wanaaza kutambua umiliki kuwa huduma rasmi na kuelewa sana ushirikiano wa washika madau rasmi. Hii njia ya chini-juu ambayo inaimarisha mfumo, kusaidia mfungamano wa mambo yalio rasmi na yasio rasmi, na ina wezesha kuelewa na kutumia kwa huduma rasmi. Njia kama chini –juu haitimizi kama njia inayotumika sana ya juu-chini, lakini inasaidia kutoa uvumbuzi wa ajabu na uwezekekano wa utendaji wa jamii. Pamoja tunafanya kazi nzuri ya kulinda watoto tukichukua nafasi zetu kama watalaam na kueleza kurahisisha utendaji wa msukomo na vile jamii ina husika kubadilika kusaidia watoto walio na changamoto.

## Shukrani

Mwandishi angependa kuwashukuru kikundi cha watafiti kutoka Sierra Leone, hasa David Lamin, Dora King, na Marie Manyeh, Sarah Lilley ambao walishirikiana na kikundi cha Global Reference na Lindsay Strak aliye ongoza kazi ya kupima matokeo.

## Marejeo

AfricanChildPolicyForum,Mtandao wa Kiafrika kwa ajili ya kuzuia dhidi ya unyanyasaji wa watoto na kutekelezwa,Mazingira na Maendeleo katika Dunia ya tatu,Huduma ya Jamii ya Kimataifa,Harakati za Afrika kwa watoto na wafanyakazi vijana,Mpango wa Kimataifa,Kikanda cha shirika la kazi kwa watoto na Ukimwi cha Team on,Kikanda la Kisaikolojia cha Kuanzisha Usaidizi,Kuokua watoto,SOS Vijiji vya watoto wa Kimataifa,Nyumba Nchini,UNICEF, & Maoni ya Dunia ya Kimataifa.(2013). Kuimarisha mifumo ya kulinda watoto kwa nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara Afrika: Wito wa Utendaji. Dakar, Sengal: Mwandishi: Ahmed. S., Al Hebshi,S., & Nylund, B.V.(2009). Sudan: Uchambuzi wa kina wa mienedo ya jamii kuhusu kutekeleza kwa ukeketaji na kutahiri wanawake (Kituo cha Makala ya kazi 2009-08) Florence, Italy:

UNICEF

Behnam, N. (2008). Kikanda, jamii na watoto: Ripoti ya Kikanda ya KuanzaKijifunza: Kuwawezesha jamii kuhusu ustawi wa watoto Watoto.Washington, DC: USAIDWashington, DC: USAID Fedha za watoto walio wakimbizi na mayatima.Inapatikana kwa mtandao. http://www.usaid.gov/ourwork/humanitarianassistance/the funds/pubs/comaction.html

Behnam, N. (2011).Shuguli mbaya: Msuguano wa mawazo, tafsiri na elimu ya haki za binadamu baada ya vita Sierra Leone (Maandiko ya udaktari ambayo haijachapishwa) Philadelphia, PA: Chuo kikuu cha Pennysylvania

Boothby,N.,Strang,A.,&Wessells,M.(Eds.).(2006).Dunia imegeuzwa juu chini:Njia za elimu ya uhusiano wa jamii na mazingira kwa watoto walio katika nchi zenye vita.Bloomfield,CT:Uandishi wa Kumarian.

Bronfenbrenner, U. (1979).Elimu ya ustawi na uhusiano wa binadamu na mazingira. Asili na desturi ya kutathmini vijiji kushiriki. Cambridge, MA: Uandishi wa Chuo Kikuu Cha Harvard.

Chambers, R. (1994). Asili na desturi ya kutathmini vijiji kushiriki. Maendeleo Duniani, 22, 953 – 969.

Kikundi cha wafanyikazi wa Kulinda watoto.(2012).Kiwango cha chini kwa utendaji wa binadamu kuhusu kulinda watoto. Geneva, Switzerland: Author.

Coinco, E. (2010). Mtazamo kwa dunia ya mimba kwa vijana nchini Sierra Leone. Freetown, Sierra Leone: UNICEF.

Collier, P., Elliott, V., Hegre, H., Hoeffler, A., Reynal Querol, M., & Sambanis, N.(2003). Kuvunja mtego wa mapigano.Washington, DC: Benki Ya Dunia.

Dagne,H.G.(2009).Uhabeshi:Uchambuzi wa ndani wa mienendo ya kutelekezwa na ya kudhuru jamii katika sehemu nne.(Kituo cha Makala ya kazi2009-07).Florence,Italy:UNICEF.

Davis, R., McCaffery, J., & Conticini, A. (2012). Kuwezesha mifumo ya kulinda watoto kwa nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara Afrika: Nakala ya kazi..Dakar,Senegal:Kikanda cha Kuwezesha mifumo katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara Afrika.

Dawes, A., & Donald, D. (2000 Kuboresha nafasi za watoto katika D. Donald, A. Dawes, & J. Louw (Eds.), Kuangazia shida za utotoni (pp.1–25). CapeTown, South Africa: David Philip.

Denov, M. (2010). Mapinduzi ya umoja wa mbele nchi Sierra Leone. Cambridge, UK: Uandishi wa chuo kikuu cha Cambridge.

Donahue, J., & Mwewa, L. (2006). Utendaji wa jamii na majaribu ya wakati: Kujifunza kutoka kwa jamii kuhusu ujuuzi na ufahamu wao. Uchunguzi wa kifani wa kuhamasisha na kuwezesha kunifaisha watoto walio na change moto nchini Malawi na Zambia. Washington, DC: USAID.

Fernando, C., & Ferrari, M. (Eds.) (2013). Kitabu kidogo cha kuimarisha

watoto walio vitani. New York: Springer

Foster, G. (2004).Utafiti wa majibu kutoka kwa Mashirika ya Kideni kwa watoto mayatima na walio na changamoto New York, NY: Mkutano wa Kideni Duniani kuhusu Amani na UNICEF.

Freire, P. (1968). Ufundishaji kwa walio dhulumiwa. New York, NY: Herder & Herder.

Graham, A., Powell, M., Taylor, N., Anderson, D., & Fitzgerald, R. (2013). Utafiti wenye maadili kuhusu watoto.Florence, Italy: UNICEF Ofisi ya Utafiti-Innocenti.

Krueger, A., Thompstone, G., & Crispin, V. (2013). Kufijunza kutoka kwa mifumo ramani ya kulinda watoto na uchambuzi katika Afrika Magharibi: Maana ya Utafiti na Sera. Sera za Kimataifa, 5, 47–55

McKay, S., & Mazurana, D. (2004). Wako wapi wasichana? Montreal, Canada: Kituo cha Kimataifa kwa Haki za Binadamu na Maendeleo ya Kidemokracia

Panter-Brick, C., & Leckman, J. (2013). Tangazo mfululizo la mhariri: Kuimarisha kwa ustawi ya mtoto- Njia zilo uganika kwa hali njema. Jarida la Saikolojia na Taaluma, Tiba ya Ungonjwa wa Akili kwa Watoto, 54, 333–336.

Stark, L., Macfarlane, M., King, D., Lamin, D., Lilley, S., & Wessells, M. (2014). Mbinu za msukumo wa jamii kwa kupunguza mimba kwa vijana nchini Sierra Leone: Tathmini fupi ya katikati London, England: Linda Watoto(Save the Children).

Thompstone, G. (2010). Mapping na uchambuzi wa mfumo wa kulinda watoto nchini Sierra Leone. Hong Kong, China: Watoto wa mpakani (Child Frontiers)

UNDP. (2013) Dalili za Umasikini na Maendeleo, Sierra Leone. Imepatikana kutoka hdstats.undp.org

Ungar, M. (2008). Ujasiri katika Tamaduni. Jarida la Uingereza ya Kazi kwa Jamii, 38, 218–235.

UNICEF. (2013). Ukeketaji na kutahiri kwa wanawake: Maelezo ya takwimu na ugunduzi wa mienedo ya mabadiliko. New York, NY: Mwandishi.

UNICEF, UNHCR, Kulinda Watoto (Save the Children), na Maono Duniani (Maona ya Dunia). (2013). Njia bora ya kuwalinda watoto wote: Nadharia na mazoea ya nfumo ya kulinda watoto, ripoti ya mkutano. New Delhi, India: Mwandishi.

Wessells, M. G. (2006). Wanajeshi watoto: Kutoka kwa Vurugu hadi Kulindwa. Cambridge, MA: Uandisi wa chuo kikuu cha Harvard.

Wessells, M. G. (2009a). Je, tunajifunza nini kuhusu kulinda watoto katika jamii? Kikanda cha mapito ya ushaidi juu ya jamii kuhusu utaratibu wa kulinda watoto katika mazingira ya kibinadamu na maendeleo. London, England: Kulinda Watoto (Save the Children)

Wessells, M. (2009b). Hakuna kufanya madhara: Kwa ajali ya taratibu

sahihi ya msaada wa kisaikolojia katika dharura za kimataifa. Msaikolojia Mwamerikani, 64, 842–854.

Wessells, M. G. (2011). Utafiti wa ethnografia/mila kuhusu utaratibu wa jamii kwa kulinda watoto na uganisho kwa mfumo wa kulinda watoto wa kitafa, nchini Sierra Leone. New York, NY: Kikundi cha Watoto walio na shida, Colombia.(Columbia Group for Children in Adversity).

Wessells, M., Lamin, D., King, D., Kostelny, K., Stark, L., & Lilley, S. (2012).Ukosefu wa uganisho, kati ya utaratibu wa msingi ya jamii kwa kulinda watoto na mfumo rasmi wa kulinda watoto kijijini Sierra Leone: Changamoto za kuanzisha mfumo madhubuti wa kitaifa kwa kulinda watoto. Watoto walio na changamoto na Masomo kwa Vijana, 7(31), 211–227.

Wessells, M., Kostelny, K., & Ondoro, K. (2014). Sababu ya kuzingatia utaratibu kwa msingi ya jamii, ya kulinda watoto na unganisho ya mfumo wa kulinda watoto ndani ya sehemu za miji mitatu na vijiji vitatu nchini Kenya: Muhtasari wa uchambuzi ulio uganishwa. London, England: Kulinda Watoto (Save the Children).

Wulczyn, F., Daro, D., Fluke, J., Feldman, S., Glodek, C., & Lifanda, K. (2010). Kubadilisha mifumu ya mbinu ya kulinda watoto: Dhana muhimu na masuala.New York, NY: UNICEF.

Zack-Williams, T. (2013). Wakati watoto wanakuwa wauwaji: Wanajeshi watoto katika vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sierra Leone. Katika C. Fernando, & M. Ferrari (Eds.), Kitabu kidogo uthabiti kwa watoto wa vita (pp. 83–94). New York, NY: Springer.